GRADI 4 -YEAR 2022
Shughuli za Kiswahili

NAME:_____

Maswali

SEHEMU 1: Mazungumzo ya ana kwa ana (Alama 5)

Kila nchi ina bendera yake maalum. Bendera husimamia mambo mengi kuhusu nchi husika. Nchi yetu ya Kenya pia twajivunia bendera yetu. Je?

1. Taja rangi zote za bendera ya taifa.
2. Bendera inapopandishwa au kushukishwa mtu hufaa kufanya nini?
3. Kifaa kipi kinachopulizwa wakati wa kupandisha au kushikisha kwa bendera?
4. Rangi nyekundu katika bendera huonyesha nini?
5. Taja maeneo mawili utapata bendera ya taifa?

SEHEMU 2: Ufahamu wa kusikiliza (Alama 4)

Msikilize mwalimu akisoma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

Sare zangu za shule zilikuwa zimechakaa. Mwalimu wa darasa aliniita na kunisihi nikamweleze mzazi wangu anitafutie sare zingine. Kwa kweli sare za shule zina manufaa mengi mno. Huwezesha kujua na kutofautisha wanafunzi wa shule tofauti. Sare pia huwafanya wanafunzi wawe na usawa. Kuna sare tofauti za kike na za kiume. Wanafunzi wa kike huvaa blauzi na sketi, marinda au suruali. Wanafunzi wa kiume huvaa shati na kaptura au na suruali.

1. Sare za msimulizi zilikuwa zime
2. Taja manufaa ya kuvaa sare za shule?
3. Wavulana huvaa sare gani?
4. Je, hapa shuleni wanafunzi wanavaa sare za rangi gani?

Sehemu 3: Kusoma kwa sauti

Soma kifungu kifuatacho kwa sauti.

Jana jioni baba alienda dukani. Alinunua sukari kwa shilingi mia moja hamsini na unga wa ngano kwa shilingi mia mbili. Aliporejea nyumbani alikuwa anatokwa na kichasho chembamba. Alipoulizwa na mama kwa nini anahema. Alisema vitu vimekuwa ghali mno. Mama alimsihi atulie ampe maji. Ilibidi nimweleze baba kuwa mambo yamebadilika. Vitu vimekuwa ghali kwa sababu viongozi hawajali wananchi.

Baba alitusihi tusome kwa bidii ili usoni tuchague viongozi wazuri. Maisha yanaweza kuwa mepesi tu kwa kuwa na elimu bora na viongozi wema. Alitupa mifano ya viongozi waliosoma kwa bidii na wema. Alituonyesha sinema zinazoonyesha kutii walimu na kuwa na bidii.